Pasteur Kitoka Moke Mutondo

KITABU CHA SHEMASI

YALIYOMO

SHUKRANI 3

UTANGULIZI 4

I. MWITO WA SHEMASI 7

I.a. Nani aliniita ? 7

2.b. Namna gani niliitwa ? 8

2.c. Niliitwa kufanya kazi gani ? 8

I.d. Je nimetumika namna inavyo nipasa? 9

I.e. Ninatumikia nini? 9

II. HALI NA TABIA YA SHEMASI 11

a) Mwenye kuokoka 11

b) Mwenye ujazwa Roho Mtakaatifu 11

c) Mwenye kujiheshimu mwenyewe 11

d) Asiye shitakiwa neno 11

e) Asiye jipendeza mwenyewe 12

f) Asiye kasirika haraka 12

g) Mukaribishaji wa watu wote 13

h) Mwenye kusamehe wengine 13

i) Mushauri na muhonyaji 14

j) Asiye kua mwoga 14

k) Mutu wa akili 14

l) Mwenye juudi 15

m) Anaye kubali kuonywa 15

n) Mwenye mke na watoto wenye kuokoka 15

o) Mwenye kuelewa maandiko matakatifu 16

III. KAZI YA SHEMASI KATIKA KANISA 18

III.1. Kazi ya mashemasi katika ibada ya kawaida na ya juma pili 18

III.2. Kazi za mashemasi katika ibada ya ubatizo 19

III. 3. Kazi za mashemasi katika ibada ya ndoa 20

III.4. Kazi za mashemasi katika karamu 21

III.5. Kazi ya mashemasi katika ibada ya meza ya Bwana 23

IV.6. Kazi zingine za mashemasi 23

Kwa mwisho 25

SHUKRANI

Katika kuandika kitabu kuusu Huduma ya mashemasi katika kanisa, tumekusudia kusaidia kundi hili la watumishi kufanya huduma yao namna inavyo mupendeza Mungu na kusaidia kanisa kuendelea mbele.
Wazo hili lilitokana na nia tunayo, kama walimu wa shule la Biblia na kwa chuo la Theologia, ya kuona utaratibu katika matumikio ya watumishi kanisani.

Kitabu hiki kilizaliwa katika shule la Biblia la magaribi pa Panzi (IBEPS / Bukavu) wakati kiongozi alituomba kufikiri jinsi ya kusaidia wachungaji kuhepuka ukosaji utaratibu katika makanisa mengi ya kiprotestante. Mbele ya kuchukua sura ya kitabu, ilikuwa somo la Diaconie et Protocole ambalo tuliwapa wanafunzi wa somo la tatu na la ine kwa shule hili. Maoni ya wanafunzi, pendekezo zao na kuvutiwa kwao kulituonyesha umuhimu ya kugeuza somo hili kuwa kitabu ambacho kitafalia hata mashemasi wasioenda kwa shule la Biblia.

Tunaleta shukrani yetu kwa Mchungaji wetu SHINDANO MASILYA ambaye anamaono mazuri ya kuona kila kikundi na kila mukristo binafsi anafanya huduma yake katika furaha na uhuru. Yeye alitusaidia kwa mashauri na alitia mukazo ili Mashemasi wa kanisa letu la 8ème CEPAC CAHI wapewe mafundisho haya.
Pia, tunamushukuru ndugu KWIGOMBA, mumoja wa wazee wa kanisa pa 8ème CEPAC CHAI ambaye alikubali kusoma na kusaihisha kitabu hiki ili kiwe na sura hii.
Mara nyingi muke wangu, Alphonsine Famba, alichukua muda kusoma na kuleta maoni yake kuusu kitabu hiki wakati alipokuwa akikiandika.

Tunafikiri, Roho Mtakatifu atasaidia kila musomaji kupata sehemu yake katika kitabu hiki na kurekebisha utumishi wake.

Pasteur KITOKA MOKE MUTONDO

UTANGULIZI

Katika 1Wakorinto sura ya 12:12, Biblia inafananisha Kanisa na mwili ambao unaweza kuishi, kukomaa na kuendelea ikiwa kila kiungo kimetumika na kufanya kazi yake vizuri. Vilevile, kwa kanisa la mahali kuendelea na kukomaa, ni lazima kila mukristo (kila kikundi) afaamu zawadi (karama) gani Roho Mtakatifu aliweka ndani yake na aitumikishe.

Shida kubwa ni kwamba wakristo wengi wanapewa huduma na madaraka kanisani, bila kufahamu kazi gani wanapashwa kufanya!. Jambo hili limeonekana hasa kwa Mashemasi ambao mara nyingi hawafuraie huduma yao na hawajui nini wanaitajika kufanya katika kanisa! .
Kwa kuwasaidia Mashemasi wetu kufahamu humuhimu wa huduma yao na nini wakristo wanatarajia toka huduma yao, tunakusudia, katika kitabu hiki kuusu huduma ya Mashemasi mambo ya fuatayo :

- Kuonyesha msingi ya huduma wa ushemasi,
- Kuonyesha ya kwamba ushemasi ni huduma sawa na zingine katika kanisa,
- Kusaidia Mashemasi kufahamu hali na tabia wanayo pashwa kuwa nayo,
- Kuonyesha kazi ya Shemasi mbele, wakati na kiisha ibada; kazi yao inje ya kanisa, na
- Kuonyesha matokeo mazuri na faida ya mashemasi katika kanisa.

Katika Matendo ya mitume 6:1-10, tunaona kwamba Wachungaji na Wazee wa kanisa wanapashwa kuhusika na mambo ya kiroho : kuhubiri, kufundisha, kuonya, kutia moyo, n.k. ; Mashemasi watausika na mambo mengine yote yasio kua ya kiroho:

- kutafuta na kuchunga vifaa vya kanisa (intendance),
- kutunza na kukinga vyombo vya kanisa,
- kusafisha na kutayarisha ofisi,kanisa na vyumba vingine vya kanisa,
- kutayarisha ibada,
- kukaribisha watu,
- kuwaketisha na kuhusika na usalama wao mbele, wakati na baada ya ibada, na kuwahudumia wakati wa karamu,n.k.

I. MSINGI WA HUDUMA YA USHEMASI

Watu wengi , wakristo na wachungaji, hawajuwi umuhimu ya huduma ya mashemasi kanisani. Kwa hiyo huduma hii inapoteza samani yake na pia nafasi yake katika ibada zetu.

Mawazo kama na haya ni mojawapo wa mambo yanayo sababisha ukosaji wa utaratibu (desordre) na manunguniko ya wakristo kanisani.

Matendo 6: 1-10 inatuonyesha kwamba Kanisa lilipo anza Yerusalemu, mitume walifanya peke yao huduma ya uchungaji na ya utaratibu katika Kanisa. Jambo hili halikua raisi kwao hata iliwabidi waache huduma ya utaratibu na wajiusishe tu na kutangaza habari njema. Ni hapa ndio huduma ya Mashemasi ilianza katika Kanisa.

Kama inavyo andikwa katika 1 Wakorinto 14: 33 Mungu wetu si Mungu wa Machafuko ila wa amani. Ndio sababu, inabidi katika kanisa utaratibu ulindwe vizuri.

Ukisoma Biblia utaona ya kwamba hata Yesu mwenyewe alikuwa mtu wa utaratibu katika huduma yake duniani:

- Wanafunzi wa Yesu walimuonyesha mwalimu wao kwamba,mbele ya kutafuta chakula cha pasaka, ni vizuri " *kutayarisha kwanza fasi pasaka ile itafanyika*"(Luka 22:9);
- Yesu vilevile aliwaonyesha wafunzi wake kwamba , mbele ya yeye kula pasaka na wanafunzi wake ni vema chakula "*kitayarishwe kwanza*"(Luka22:8);
- Yesu alifahamu ya kwamba , mbele ya kugawa mikate kwa watu elfu tano," *ni lazima kuwe watu (wanafunzi wake) watakao ketisha mkutano*"(Luka 9:14);
- Yesu alionyesha kwamba " *si kila mtu ndie anapashwakujitwalia mikate ao kuyagawa, ila ni kikundi fulani cha watu (wanafunzi wake) ndio wanapashwa kufanya kazi hii ya kugawa mikate*" (Luka 9:16);
- Yesu alionyesha pia kwamba "ni *lazima chakula na vyombo vinavyo baki baada ya kula vichungwe vizuri*"(Luka 9:17);
- Biblia inaonyesha kwamba "*ni lazima hotuba itamkwe vizuri kusudi waalikwa waelewe kusudi na utaratibu karamu*" (Luka 22:15-23);
- Biblia inaonyesha kwamba "*ni lazima wenye kugawa chakula wafaamu kutuliza na kuwatia moyo wenye kunungunika wakati wa karamu*"(Luka 22:26-30);
- Biblia inaonyesha kwamba ni muhimu kanisa liwe na watu "*watakao husika na kugawa chakula*"(Mdo 6:2).

Maandiko haya na mengine yatuonyesha kwamba huduma ya Mashemasi ina msingi wake, sio katika mawazo ya wanadamu, ila katika maandiko matakatifu.

Ulizo la muhimu tunaloweza kujiuliza ni lile la kufahamu ikiwa ushemasi ni huduma ao hapana na ni wanani wanapashwa kuifanya.

Maandiko matakatifu yanatuonyesha kwamba kila huduma katika kanisa inafanyika kufuatana na karama kila Mkristo anakua nayo. Kwa hivyo ni lazima tufaamu kwamba si kila mkristo ndiye anaweza kutajwa kuwa shemasi; ila ni wale tu ambao Mungu aliwajalia neema na kuwapa karama hii.

Kwa hivi ushemasi unastahili kuheshimiwa na watu wote kwa sababu ni huduma sawa na uchungaji, uimbaji, n.k. Shida ni kuona kwamba katika makanisa yetu leo Mashemasi wanazarauliwa na kukamatwa sawa watumwa wasio stahili mushahara na heshima yoyote !.

Ni lazima kwa wachungaji, wazee, na wakristo wote wafaamu na kuelewa kwamba shemasi anajukumu kubwa sana katika kuendelea kwa kanisa la mahali. Wasipo safisha kanisa , wasipo karibisha watu vizuri, wakikosa hekima katika kupanga watu, wakigawa chakula kwa upendeleo,watu hawata sikiliza mafundisho kwa furaha,wengine watakimbia, na karamu haita fanyika kwa salama na umoja !
Ndio sababu shemasi,kwa umuhimu wa huduma yake anaitajika kuwa mtu mwenye Mwito,karama na mwenendo bora, yaani mtu aliye itwa na Mungu, anaye ongozwa na Roho Mtakatifu.

I. MWITO WA SHEMASI

Mwito ni neno la lazima na la kwanza katika maisha ya kila mkristo kwa jumla na kwa maisha ya Shemasi kwa binafsi ikiwa anapenda kufanya huduma yake vizuri na kuzaa matunda.

Kwa hivi, mbele ya kukubali kuombewa kuwa shemasi, ni lazima mukristo ajiulize ikiwa anamwito wa kuwa shemasi ao hapana. Ndio sababu shemasi anaitajika kujiuliza maulizo sita kuusu mwito wake.

I.a. Nani aliniita ?

Magomvi na kelele nyingi yanayo tesa kanisa leo yanatokana na namna mbalimbali ambazo watumishi wengi waliitwa kufanya huduma kanisani.

Ni lazima tuonyeshe ya kwamba kunawatu wengi wanapewa huduma sio sababu wanamwito toka Mungu lakini wana mwito wa kimwili. Ndio sababu tunakuta:

- Kuna walio itwa na jamaa zao,
- Walio itwa na marafiki zao,
- Walio itwa na tamaa yao, na kuna
- Wale walio itwa na Mungu mwenyewe.

Lakini, kwa shemasi kuwa mtumishi anaye faa kwa Mungu na kwa kanisa, ni lazima ahakikishe kwamba aliitwa na Mungu peke yake na yakwamba kazi zote anazo zifanya anazifanya kwa kumupendeza Mungu aliye muita. (1 Kor 1,1).

Ulizo hili liliwasaidia sana Musa na Mtume Paulo kufaulu katika utumishi wao. Ndio sababu Mtume Paulo alianza kuandika barua zake katika kuonyesha ni nani alimwita kua Mtume : *Paulo, Mutume (si wa watu , wala kwa mutu , ila kwa Yesu Kristo na Mungu Baba aliye mufufua toka wafu).*

Kufaamu nani alimuita kutamusaidia Shemasi kuwa na utumishi bora unao mupendeza Mungu na kujenga kanisa.

Sababu walijua ni nani aliwaita, Musa na Paulo walipata jibu kwa matatizo walio kutana katika utumishi wao:

- Wakati Musa alipata shida ya kuvusha wana wa Israeli bahari nyekundu, aliposhambuliwa na ndugu zake kwa kukosa chakula , taifa lingine lilipokuja kumupiganisha, Musa hakulalamika wala kuomba msaada kwa ndugu zake wala hakumwita baba mukwe wake Yetero amutetee; lakini alimukimbilia Mungu peke yake ,sababu alifahamu kwamba si ndugu zake wala Yetero ndio walimuita akombowe wa Israeli (Kutoka 14:10-14;15:22-27;16:1-11) .
- Paulo na Sila walipo tupwa gerezani baada ya kupigwa uchi sokoni, Paulo hakutuma watu wamwite Anania aliye muwekea mikono aje awateteye; lakini, usiku wote walikesha wakimwimbia na kumuabudu Mungu aliye waita (Mdo 15:22-40)

- Katika utumishi wao, Musa na Paulo walitafuta kumupendeza Mungu, kuliko kupendeza wanadamu ambao hawakuwafanya kuwa watumishi.
- Katika utumishi wao Musa na Paulo walitafuta tu sifa na faida ya Mungu aliye waita, sio sifa wala faida yao wenyewe ao ya jamaa zao.

Vilevile, Shemasi anaitajika kuwa na uwakika wakuitwa na Mungu; kama sivyo, inamubidi aache na angoje siku Mungu ataweka karama iyo ndani yake.

2.b. Namna gani niliitwa ?

Ni muhimu sana kila mtumishi kanisani kuelewa namna gani aliitwa. Wakati Mtume Paulo anapo jitaja kuwa Mtumishi kwa mapenzi ya Mungu (1Kor.1:1a) anapenda kuonyesha Unyenyekevu katika utumishi wake. Ndio sababu hata Bwana Yesu mwenyewe alichukua maji na kuwanawisha wanafunzi wake(Yn 13:1-12)

Mashemasi wengi wanakosa unyenyekevu sababu hawafahamu ya kwamba wao ni mashemasi kwa *Neema ya Mungu peke yake* , ila si kwa sababu ya kimo chao, mali yao, ujuzi wao,n.k..

Ni lazima kila shemasi afaamu kwamba ni kwa Neema ya Mungu ndiyo anakua ginsi alivyo na yote anayo yafanya anapashwa ayafanye katika kunyenyekea sio kwa kiburi na majivuno, hivyo akitarajia kupokea taji ya uaminifu katika mikono ya Bwana wa kazi.

Tunaona mashemasi wengine wanajivuna na kukataa kufanya huduma yao kanisani. Nilazima wafaamu kwamba Mungu anaweza kuondoa huduma ile ndani yao na kuipatia wengine. Biblia inaonyesha wazi hatari ya kiburi na kukosa unyenyekevu : kiburi ni mwazo wa anguko (Mezali 15 : 33), kila mwenye kujishusha kama mtoto mdogo, atakuwa mukubwa katika ufalme wa mbingu (Matayo 18 : 4); aliye mukubwa kati yenu, atakuwa mutumishi wenu (Matayo 23 : 12).

Hali hii ya kunyenyekea lilimusaidia pia Paulo kuwa kiongozi mutumishi pahali pa kuwa kiongozi mukubwa kuliko wengini wote (Ro 12:3 ;1Kor 4:7;1Kor 15:10-11)

2.c. Niliitwa kufanya kazi gani ?

Neno la tatu kila shemasi anaitajika kufaamu kuusu mwito wake ni kazi aliyoitiwa kufanya katika kanisa. Tumeshangaa sana kuona ao kusikia Shemasi anaitaji naye aombewe kuwa Mzee ao Mchungaji wa kanisa !

Haiwezekane Shemasi afae kabla hajaelewa kwamba ni ile huduma Mungu alimuita kufanya na aifuraie akimushukuru Mungu kwa kumufanya kuwa shemasi. Hii itamusaidia kuhepuka uvuguvugu na wivu katika utumishi wake.

Mtume Paulo, ijapokuwa ni yeye alifunguwa makanisa katika Azia , hakujifanya Mchungaji wa kanisa la mahali, wala hakuusika na kugawa chakula na misaada mbalimbali ;sababu alijua kwamba *Mungu alimuitia kutangaza habari njema* (Evangéliste) *peke yake* na huduma zingine zitafanyika na wakristo wenye kua na karama hizo (Ro 1:1c).

Ni lazima kila Shemasi atosheke na huduma yake na aifanye kwa furaha bila kutamani ya wengine. Hii ni njia nzuri ya kupendeza Mungu na kuwa faida kwa kanisa lote.

I.d. Je nimetumika namna inavyo nipasa?

Kuchunguza namna anavyofanya huduma yake katika kanisa ni neno la Ine la kufahamu katika mwito wa Shemasi. Kufanya kazi kwa manunguniko, kwa kusukumwa ao kwa zoezi ni mwanzo wa kuharibika kwa huduma ya wakristo wengi katika kanisa.

Mtume Paulo alipiga vita vyema na kumaliza mwendo wake katika furaha na ushindi, sababu alijua kuchunguza nini nimekwisha kufanya,wapi nimekwisha fikisha Habari Njema na wapi sijafikisha (Ro 15:19). Ni muhimu sana kwa Shemasi kuchunguza namna gani anavyo hudumia, ikiwa anafanya kazi yake vema hao vibaya.(1Tes. 2:2; 2:8; Fil 2:18).
Nabii Yeremia anaonyesha wazi hasara ya kufanya kazi ya Bwana kwa uzaifu ao kupuuzia : Kuna laana inayo fuatana naye (Yeremia 48 : 10a).

I.e. Ninatumikia nini?

Kujua kujitoa ni ya lazima sana katika huduma ya Shemasi, sababu anaitajika kuhudumia watu wengi kila mara anapoitajika, sababu mapokezi yao huandaa watu kupokea baraka kwani ushugulikiwa vizuri.
Lakini mara nyingi si raisi kuona Mashemasi wanajitoa bila manunguniko wala uzaifu; hali hii mbovu inatokana na mambo matatu:

- Katika makanisa mengi wachungaji na wazee wanakua na mishahara kwa kazi wanazo zifanya; lakini mashemasi hawapewi chochote
- Mara nyingi katika mikutano mbalimbali ao katika kanisa la mahali, mashemasi hawatiwi moyo kwa kazi wanazo zifanya ; mapastori na wakristo wengine hawajue kusema Asante baada ya kuhudumiwa na Mashemasi ;
- Mara nyingi watu huzarau Mashemasi na kukataa kutii utaratibu katika kanisa, karamu, kama ulivyo
- pangwa na Mashemasi !

Hali hizi tatu zina wasukuma mara nyingi Mashemasi (wasioelewa mwito wao) kujiuliza: Tunasumbukia nini ao tunatumikia nini?
Ulizo hili silo mbaya ,sababu hata Mtume Petro alimuuliza Bwana Yesu nini atapokea baada ya kumufuata Yesu (Matayo 27). Ila tufaamu kwamba ulizo hili ni la Mashemasi wanaotafuta faida yao wenyewe na ambao hawawezi kutafuta faida ya wengine (Fil 1:21). Mashemasi kama hawa wanakubali kuitwa Mashemasi wakati wa furaha tu.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatoa jibu kamili na nzuri kwa ulizo hili :*kwa sababu Mungu si muzalimu hata kusahau kazi yenu (Wae 6:10a)* . Bwana Yesu vilevile alimuonyesha Petro kwamba yeyote anaye kubali kumtumikia atapata faida mbili kubwa : *atapokea mara dufu hapa duniani na mbinguni atapata uzima wa milele.*

Sio rahisi kwa mwanadamu kuelewa na kushuhudia ukweli wa jibu hili la Yesu; ila jambo hili limetendeka katika maisha ya Mashemasi : *wao wasio na mshahara, wanalisha jamaa zao, wamesomesha watoto wao na hata mumoja wao hatembei uchi.*

Kwa hivyo, nilazima Mashemasi waelewe kwamba kazi wanayo ifanya si ya bure ,sababu Mungu aliye waita na wanaye mtumikia atawalipa nakubariki jamaa zao na kamwe hata waacha kupata haya (2 Watesalonika 2: 25). Kumbe , pahali pa kuvunjika moyo wajipe moyo .

II. HALI NA TABIA YA SHEMASI

Sio mwito peke yake ndio inaweza kumusaidia Shemasi
kufuraiwa na watu wote katika huduma yake; ila tabia na hali yake vilevile ni ya muhimu. Ndio sababu shemasi anaitajika awe :

a) Mwenye kuokoka

Haiwezekani shemasi awe na utumishi bora ikiwa yeye bado kuzaliwa mara ya pili ; yaani kumwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake binafsi na kumwacha Roho Mtakatifu kuongoza maisha yake.

Mtume Paulo alionyesha umuhimu wa mwanadamu kuachana na mutu wazamani na kujivika mtu mupya. Ndio sababu ameandika: Kwa *sababu kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa lakini kiumbe kipya* (Gal 6:15).

Shida kubwa ni kwamba watu wengi wameombewa ushemasi si kwa sabasu wameonekana wameokoka lakini hakose wao ni ndugu, rafiki ao jirani wa Mchungaji. Matokeo ni mabaya hadi kufikia kuwa na Mashemasi wenye kiburi, wenye kujipendelea, wevi, washerati, wenye kuchafua kanisa nzima na wenye kukimbiza wengine pahali pa kuwavuta kwa Kristo!

b) Mwenye ujazwa Roho Mtakaatifu

Ni lazima Shemasi awe mtu mwenye kujazwa Roho Mtakatifu; sababu huduma yake sio ya kimwili ila ni ya kiroho.

Wagalatia sura ya 5 na haya yake ya 18 inaonyesha kwamba bila kujazwa Roho Mtakatifu, hatuweze kushinda tamaa za miili yetu.Hali hii iliitajika kwa mashemasi wa matendo 3:6.

c) Mwenye kujiheshimu mwenyewe

Shemasi anastaili kuwa mtu mwenye kujiheshimu; sababu huduma yake haimuruhusu kuwa na tabia za kufanya mizaa na watu, kusema uwongo ao kuvaa mavazi yasio faa, kula kwa tamaa, n.k.

Mara nyingi shemasi anafananishwa na mtu wa protocole katika serkali, akiwa mtu wa mizaa hakuna atakaye fuata na kutii utaratibu anayo stahili kuweka katika ibada, karamu ao kusanyiko yoyote!

d) Asiye shitakiwa neno

Shemasi, kama mukristo anayehusika na utaratibu, usalama, kuchunga vifaa, kugawa chakula na kutumwa, anapashwa kuwa mtu mwenye kuaminiwa na watu wote. Huduma ya mashemasi wengi umeharibika na kuzarauliwa sababu ya ushuhuda wao mbaya:

- wamoja wameshitakiwa kuiba vyakula wakati wa karamu,
- wengine hustakiwa uzinifu,
- wengine upendeleo,

- wengine hustakiwa madeni za watu !

Kwa kuhepuka kuwa na mashemasi wanao laumiwa, Mtume Paulo anamushauri Timoteo kwamba na hawa (mashemasi) wajaribiwe kwanza; kisha watumike kazi ya utumishi kama wakiisha kuonekana pasipo kosa (1Tim 3 : 10).

Nabii Samweli anakuwa mufano muzuri wa ushuhuda ambao mashemasi wanatajika kuwa nao: mbele ya kuacha uongozi wa taifa la Israeli na kumushimika Saulo kama kiongozi mupya, alialika waisraeli wote na kuwauliza: *mimi ni hapa, mushuhudu juu yangu mbele ya Bwana, na mbele ya mupakaliwa wake (Saulo), ni ngombe ya nani niliye mutwaa, ao punda ya nani niliyo itwala, ao nimedanganya nani, nimetesa nani, ao nimepokea rushwa kwa mukono wa nani inipofushe macho, nami nitawarudishia ninyi.*

Ila watu wote walimujibu: *Hukudanganya mutu, wala hukutesa wala hukupokea kitu toka kwa mukono wa mutu* (1 Sam 12:3-4).

Ni lazima kila Shemasi awe na ushuhuda muzuri kusudi kupitiya ushuhuda wake watu wavutwe kwa Yesu na wamutukuze Mungu.

e) Asiye jipendeza mwenyewe

Kama tulivyo sema kuusu mwito wa shemasi, unyenyekevu ni ya muimu sana katika maisha yake. Kiburi, majivuno na majitapo imekua jaribu kubwa katika huduma ya shemasi, hata wengi kati yao wanazani pasipo wao hakuna kinacho weza kufanyika katika kanisa!

Tabia kama na hii sio nzuri ,sababu mashemasi wanaitaji kufahamu kwamba wao ni vyombo tupu ambavyo Mungu anatumia na kwamba Mungu anaweza kutumia wengine pahali pao.

Mtume Paulo anaonyesha mufano muzuri wa kutokujipendeza mwenyewe wakati wakristo wa Korinto wanagombana mpaka kujigawa kwa vikundivikundi. Japokua alikua Mtume na Apolo hakuwa Mtume, hakujipendeza kuwa wa lazima kuliko Apolo, wala hakujitapa kufanya kazi kuliko Apolo; ila alisema :*Basi Apolo ni nani, na Paulo ni nani ? ...Mimi*

Nilipanda, Apolo akatia maji, lakini Mungu alikuza (1Kor 3 :5a; 3 :6 soma pia Rom 15 :1b). Mashemasi wanapashwa kuiga mufano wa Paulo aliye jizuiza na kujisifu wala kujitapa kwa kazi aliyo ifanya kwa Neema ya Mungu.

f) Asiye kasirika haraka

Huduma ya ushemasi inaitaji uvumilivu mwingi sana, sababu kazi yake inamufanya kuwa mutumishi wa watu wengi hata wa wale asiyo wajua. Kwa hivyo imemubidi asiwe mtu wa kukasirika haraka.

Mara nyingi kanisani munaingia watu wa kila haina : wapagani, wakristo wachanga, maskini,matajiri, wenye kutoka katika jamaa za walevi , wenye kujipenda kuliko wengine, makahaba,

wenye kiburi,wanyenyekevu, n.k. ; na ni Shemasi ndiye anapashwa kuwakaribisha na kuonyesha kila mumoja wapi atakaa. Jaribu ni kwamba wamoja hawata tii maongozi yake na kwenda kukaa fasi Shemasi hakumuruhusu kukaa ! Ao kuna mara katika
karamu, watu wengi wanapenda wapate chakula mara mbili japokua watu wote hawaja kula ,wengine hupenda kupeleka chakula katika jamaa zao, wengine huleta watoto kwa karamu na kupenda watoto wao wapate chakula mbele ya waalikwa !
Mbele ya jaribu kama hizi na zingine, Shemasi anaitajika kuwa mutu wa moyo na kusaidia watu kuelewa mambo kwa sauti ya upole akiwaonya kwa upendo

Ndio sababu Mtume Paulo anatuonya sisi tulio na nguvu kubeba uzaifu wao wasio na nguvu.(Rom 15 :1) yaani tunapashwa kuwavumilia, kuwaelewa na kuwasaidi kukomaa ao kua na nguvu.

g) Mukaribishaji wa watu wote

Shemmasi hastaili kuwa mtu wa upendeleo wala wa ubaguzi : anapashwa kukaribisha na kuhudumia watu wote sawa.
Wakati Shemasi anatumia upendeleo katika huduma yake, anaweka kanisa mbele ya hatari Ine:

- Anapanda chuki kati ya wale anao wapendelea na wale asiye wapendelea,
- Anapenda wale anao chukia waondoke katika kanisa ,
- Anaonyesha kwamba upendo unao hubiriwa kanisani ni wa uwongo,
- Anapanda manuguniko ndani ya mioyo ya wale anaowachukia.

Habari ya Bwana Yesu na muke wa Zebedayo inatufundisha mengi kuusu hatari ya upendeleo : Yesu asingetumia hekima ya uMungu wake, angeliweza kupata shida ya kuona wanafunzi wake kupigana, kugombana ao wengine wasio kuwa wa jamaa lake kumuacha na kurudi kwao: Salome, sababu alikuwa dada ya Maria mama wa Yesu ,alipenda kuleta ubaguzi na upendeleo wa kindugu katika huduma ya Yesu wakati alipo muomba : *Amuru hata wana wangu hawa wawili (Yakobo na Yohana) waketi,mumoja kwa mukono wako wa kuume ,na mumoja kwa mukono wako wa kushoto, katika ufalme wako.*(Matayo 20 :20-21). Ombi hili la Salome lilileta manunguniko kati ya mitume hata kuwaleta wale wasio kuwa ndugu wa Yesu kimwili kujiuliza, sasa sisi , nani atatutetea nasi mbele ya Bwana? . Yesu asingeli vumbua mawazo yao na kuwaonya, upendeleo na ubaguzi huu wa Salome ungelete shida!
Kanisa nyingi yameharibika na kuchafuka leo sababu ya tabia ya ubaguzi na upendeleo !

h) Mwenye kusamehe wengine

Shemasi hapashwe kuwa mtu wa kuchunga hasira ao roho mbaya; sababu asije akamupe shetani nafasi katika utumishi wake.
Katika kitabu cha Walawi 19: 18, Mungu anawaonya wa Israeli wasiwe na chuki, wala wasilipishe kisasi kwa jirani zao.

Shemasi anapashwa, wanapo mkosea, kuwa tayari kusamee kusudi yule aliye mkosea atambue ndani ya Shemasi ukuu wa kazi Yesu alifanya msalabani.

i) Mushauri na muhonyaji

Huduma ya Shemasi inamuomba awe mtu mwenye kujua kushauri na kuonya wengine.
Kama tulivyosema hapa juu, Shemasi anakutana na watu wa kila aina na wengi kati yao wanaitaji kuonywa na kushauriwa: wamoja wanapenda kukataa chakula katika karamu, wengine wanajiona kuwa bora kuliko wenzao, n.k.. Ndio sababu Mtume Paulo alimuomba Timoteo awe tayari kuhamakia wale wote wanao tenda zambi katika kanisa kusudi wote waishi katika amani na salama.(1 Tim 5:20).

Neno kubwa na la lazima ni kufaamu kusudi la maonyo katika kanisa : *ni kusaidia wazaifu kukomaa kiroho*; ndio sababu maonyo ya shemasi inapashwa kufanyika katika upendo .Ikiwa Shemasi hajue kuonya na kushauria , kanisa haliweze kuendelea ;sababu, kama hajue kukaribisha watu na kuwasaidia kuelewana , na kuheshimiana, watu wote wataishi katika uvuguvugu.

j) Asiye kua mwoga

Shemasi, kama mtu anaye usika na usalama, hastahili kuwa mwoga. Ni haibu sana kusikia ao kuona mulevi ao mwendawazimu anaingia na kuleta fujo katika kanisa!
Kuwepo kwa mashemasi katika kanisa, inapashwa kuleta uhakika kwa watu kwamba hakuna mutu anayeweza kuchafua usalama katika kanisa.
Mara nyingi tunaona watu wanapigana katika karamu; ni lazima shemasi awe tayari kuamua na kuachanisha.
Shemasi ni mtumishi wa upatanisho, sababu anakaribisha hata maadui wake, maadui wawili na kuwasaidia kuishi pamoja; pia shemasi anasikia habari nyingi hata za hatari .Kwa hivi anaitajika kuwa mtu wa maombi sana akimuomba Mungu amupe moyo wa ujasiri na uhodari.
Pia, mara nyingi Mashemasi wanaitajika kuwasaidia wagonjwa na kuwapeleka kwa muganga ao kwa waombaji, inamubidi basi asiwe wa kwanza kuogopa hali ya mugonjwa, ila anapashwa kuwa tayari kumutia mugonjwa moyo akimusaidia kuweka tumaini lake katika Kristo.

k) Mutu wa akili

Shemasi anapashwa awe mutu wa akili, sababu inamubidi kusikia habari toka kila mtu, kuonywa na watu , kusikiliza mawazo ya watu wa kila aina . Kwa hivi, imemubidi awe na uwezo wa kuchunguza habari hizi, mawazo yote na kujua ya wapi inaweza kubomoa kanisa na ya wapi inaweza kujenga.

Vile vile katika kugawa chakula, mavazi na vinginevyo imemupasa Shemasi atumie akili.

Ndio sababu Mtume Paulo anasema: *Basi ni nini ?, nitaomba kwa Roho, na nitaomba kwa akili vilevile ;nitaimba kwa Roho na nitaimba kwa akili vilevile* (1Kor. 14 : 15). Katika maandiko haya Mtume Paulo anaonyesha kwamba kuongozwa na Roho Mtakatifu hakuweze kumuzuia Mtumishi wa Mungu kutumia akili kwa utukufu wa Bwana.

l) Mwenye juudi

Katika kanisa ,sio Mchungaji tu ndie anaitajika kuwa mtu wa juudi; ila Shemasi vilevilie haweze kuweza huduma yake ikiwa hana juudi : ni yeye anahusika na usafi katika kanisa ; japokua watu wengi huingia kanisani na matope baada ya Shemasi kusafisha. Shida kubwa ni kuona watu wengi hawafaamu kwamba ni lazima kwao kuheshimu kanisa sababu yule anaye weka usafi ndani ni mwanadamu kama na wao.

Juudi ni neno la lazima katika maisha ya Shemasi, kwa kuwa anaweza kurudilia kazi moja hata mara nyingi kwa siku moja : anaitajika kufika wa kwanza kanisani na atoke wa mwisho; anaitajika kuwapa watu zaidi ya mia moja chakula, maji na kutengeneza vyombo baada ya karamu.
Mtume Paulo anakuwa mufano muzuri wa juudi, baada ya kutangaza habari njema katika Galatia, maadui wa Injili walifika na kubomoa mafundisho aliyo yaacha pale; lakini japo hivyo, Paulo hakuchoka kuwashahuri hata kupitia baruwa (Wagalatia 1 : 6-10).

m) Anaye kubali kuonywa

Imemupasa Shemasi awe mtu mwenye kukubali kuonywa, kwa hivi anaitaji kusikiliza kila mtu bila kuzarau hata mutu mumoja, hata kama yeye ni mtoto ao maskini.

Biblia inaonyesha waziwazi hatari ya kukataa kuonywa :*Yeye anayeonywa mara nyingi na anafanya shingo yake ngumu anavunjika gafula, pasipo njia ya kupona*.(Mezali 29:1).
Huduma ya shemasi haimuruhusu kua mtu asiye kubali kuonywa, sababu anapashwa kufanya kazi yake katika hekima. Kwa hivi anaitaji kufunzwa kila siku ya maisha yake. Mwandishi wa kitabu cha Mezali anaonyesha pia uhusiano kati ya kukubali shauri na hekima : *Lakini mwenye hekima usikiliza shauri* (Mezali 12:15b).

Mara nyingi tunawaona mashemasi wanashindwa kugawanya chakula kwa watu wote , kupanga watu vizuri sababu ya kukataa kupokea mashauri ya watu wengine.

n) Mwenye mke na watoto wenye kuokoka

Imemupasa Shemasi awe mume wa muke mwenye kuokoka na baba wa watoto wenye kuokoka. Huduma yake , kama tulivyo sema, inamuomba Shemasi awe mtu mwenye kujitoa ; kuna mara muda wake

mwingi ataupitisha kwa kanisa, kuna mara atatoa mali yake kutafuta vifaa vinavyo kosa kusudi karamu ifanyike vizuri, kuna siku ataitajika kulala inje ya nyumba yake ao kurudi nyumbani nyuma zaidi , n.k.
Imemubidi basi muke wa Shemasi asiwe na wivu sana na awe tayari kumushauria mume wake ao muke wake (sababu kuna wanawake wenyekua pia na karama ya ushemasi) kusudi huduma ya ushemasi ifanyike katika furaha.
Neno la lazima ambalo wake ao waume wa mashemasi wanaitajika kufaamu ni kwamba mara nyingi mashemasi wanarudi nyumbani na maneno mengi katika mioyo yao : wamoja wamerudi na hasira, wengine wamerudi wamevunjika moyo ;wengine wamerudi wamechoka na wanaitaji kusaidiwa, sio kimwili tu ila kiroho vileviile.

Shauri la muke wa Pilato kwa mume wake kwa ajili ya mastaki ya Yesu, ni mufano unao stahili kufatwa na wake ao waume wa mashemasi: *Usiwe na neno na mtu huyu mwenye haki (*Matayo 27: 19c).

Shauri hili la muke wake lilimusaidia kunawa mikono yake na kukiri kwa kinywa chake kwamba Yesu hana kosa lolote.

Ikiwa watu wa nyumba ya Shemasi hawaokoke wanaweza kuwa kwazo kubwa kwa huduma yake. Tume kwisha kuona wake wamashemasi wenye kuhamakia waume wao sababu wamewaona wakifyagia ao wakikoropa katika kanisa! ; na hii inawaletea shida sana wakishindwa kuamua nini watii kati ya mwito na matatizo ya jamaa.

Japo kuwa tunatia mkazo kwa wokovu ya watoto wa mashemasi, hatusahau ya kwamba mara nyingi shemasi analaumiwa ikiwa watoto wake ni wapagani; lakini, wanapojitowa wote kwa kazi ya Mungu, wengine huwaza mashemasi wanatayarisha watoto wao kuwakomboa katika huduma.
Neno hili linakuwa jaribu kubwa ambalo linawavunja mashemasi wengi moyo!

Pamoja na huduma anakuwa nayo kanisani, Shemasi anapashwa pia kuwa na mda wa kuhusika na jamaa lake. Mashemasi wengi wanaachilia jamaa zao na ndio sababu wake wao na watoto huchukia Kanisa ambayo inashababisha mume wao ao baba yao kuwa achilia.

Ni lazima kwetu kuonyesha kwamba japokua muke, mume na watoto wa Shemasi wameokoka, sio lazima kwa Shemasi kuwatumia katika kutimiza mapashwa ya huduma yake . Sio vema Shemasi kutuma muke wake kusafisha kanisa pahali pake, sababu huduma ni yake na Mungu aliye muita atapima matendo yake. Sio vema huduma ya shemasi kua jaribu kwa jamaa lake.

o) Mwenye kuelewa maandiko matakatifu

Imemupasa Shemasi awe mtu mwenye kuelewa maandiko matakatifu, sababu mara nyingi anapata muda wa kuzungumuza na wageni wakati wa kuwahudumia. Haimupase tu kuwauliza majina yao, mahali wanapotoka, zehebu wanazo shiriki, na huduma wanazo zifanya katika zehebu zao; ila anapashwa

pia kujibu kwa maulizo yao ya kiroho, kuwazungumuzia habari ya upendo wa Mungu kwa vinadamu na faida ya kumupokea Yesu katika maisha yao.
Ndio sababu Mtume Paulo anamuhonya Timoteo kwamba ni lazima mashemasi wawe wakishika siri ya Imani katika zamiri safi (1 Tim 3:9).

Hakika, sio vyepesi kutaja tabia na hali zote ambazo Shemasi anapashwa kuwa nazo katika kitabu, sababu hali yake inapashwa kupatana na mahali alipo(kanisani, njiani, nyumbani), huduma anayo hifanya(kusafisha kanisa, kuhudumia kwa karamu, kwa maziko, n.k.).

Lakini kati ya hali zote zinazoitajika kwa Shemasi ya lazima kuliko zote ni kuzaliwa mara ya pili na kuacha Roho Mtakatifu kuongoza maisha yake. Pasipo hivi, haiwezekane Shemasi awe mtumishi anaye faa kwa Mungu na kwa kanisa.

III. KAZI YA SHEMASI KATIKA KANISA

Baada ya kuona habari za mwito , hali na tabia za Shemasi, ni lazima kwetu kujibu kwa ulizo Shemasi atafanya kazi gani katika kanisa ?. Ulizo hili ni la lazima sana kwa kitabu hiki , sababu jibu lake litasaidia mashemasi wetu kutumika kazi yao pahali pa kutamani ya Wazee, ao ya Wachungaji. Japokuwa mashemasi wanaitwa watumishi, ni lazima tufaamu kwamba wao si watumishi wa Mchungaji binafsi ao wa wazee wa kanisa; ila ni watumishi wa Mungu katika kanisa. Maana yake, kila kazi mashemasi wamefanya inapashwa kufanyika kwa utukufu wa Mungu kwa jina la kanisa. Inawezekana mashemasi ku hudumia watumishi wengine kwa kujengana kiroho, lakini si vizuri muchungaji kuwachukuwa kama wafanyakazi wake.

Sababu hii, tutaona kazi za mashemasi katika Ibada mbalimbali, katika siku kuu za kanisa na katika sherehe zenye kuandaliwa na kanisa.

III.1. Kazi ya mashemasi katika ibada ya kawaida na ya juma pili

Mashemasi wanakuwa na kazi kubwa ya kufanya kusudi watu wote wanao ingia katika ibada ya kawaida (la kati ya juma) na ya jumapili (siku ya Mungu) wafurai na kujisikia huru kuimba, kusikia neno la Mungu na kumuabudu.

Ni huzuni kuona mashemasi hutia mkazo kwa ibada ya juma pili na kuzarau ibada ya kati ya juma ao kuona mashemasi huwaza kwamba huduma yao huanza wakati watu wanaanza kuingia katika kanisa ! Tabia ao mawazo haya si sawa na inasababisha kuzorota kwa huduma yao. Ndio sababu tunawajulisha kwamba huduma yao inapashwa ifanyike mbele, wakati ya ibada na baada ya ibada.

a) Mbele ya Ibada

Siku moja mbele ya ibada , mashemasi wanapashwa kuanza kazi ya matayarisho ya ibada na kuwa na uwakika kuusu:

- Usafi wa kanisa na kandokando yake
- Kupangwa kwa viti vizuri kufuatana na mpango wa ibada:
  kujua nani atakaa wapi na atakaa ku nini
- Usafi wa nguo zote zitakazo tandikwa katika ibada (juu ya meza, juu ya viti, juu ya vyombo fulani)
- Vyombo vya kwaya ni vingapi na vitakaa wapi
- Gari za wenye watakao kuja kanisani zitakaa wapi, nani atausika na kuzipanga, nani atalinda usalama wa gari zinyewe
- Kutayarisha maji ya kunywa kwa watu
- Kuchunguza hali ya viti ikiwa ni nzuri hao hapana (kujuwa vyenye kuvunjika na kuvitoa inje)
- Kupanguza viti watu watakavyo ikali
- Kutafuta mahuwa na kuyapamba katika kanisa

- Kutayarisha vikapo vya kutolea sadaka
- Kusafisha mahali pa choo kubwa na ndogo

b) Wakati wa ibada

Baada ya kujuwa nani atafanya nini mbele ya ibada na kutayarisha vifaa vyote vya lazima kwa ibada, inawaomba mashemasi , wakati wa ibada :

- Kukaribisha watu kwa milango mbalimbali ya kanisa,kuwapokea ndani ya kanisa, kuwaketisha katika kuwapanga
- Kuhusika na kurahisisha mawasilioano kati ya watu ndani ya kanisa kutoa baruwa kwa mumoja na kuifikisha kwa mwengine
- Kuwapokea na kuwapanga vizuri wenye wanakuja kwa musalaba, na kuwaongoza wapi watakwenda baada ya kuombewa
- Kuwaongoza wale wanao itaji kwenda kwa lazima kubwa ao ndogo

c) Baada ya ibada

Ni lazima mashemasi waelewe kwamba ni wao wanapashwa kuondoka nyuma ya watu wote katika ibada , sababu wanapashwa :

- Kurudisha kila chombo maali pake baada ya ibada
- Kuchunguza kitu gani kiliweza kusaulika katika kanisa na kukilinda vizuri
- Kupanga viti vizuri na kuchunguza ikiwa kunakiti kilicho haribika iliwatoe ripoti ya kukitengeneza
- Kuondoa uchafu ulioachwa na watu katika kanisa
- Kufunga milango ya kanisa
- Kuwapa maji wale wenye kuwa na kiu.

III.2. Kazi za mashemasi katika ibada ya ubatizo

Sio wachungaji , wazee na waimbaji tu ndio wanakuwa na kazi ya kufanya katika ibada ya ubatizo; ila mashemasi pia wanakuwa na kazi kubwa na ya muimu wanayo itajika kuifanya mbele,wakati na baada ya ibada hii.

a) Mbele ya ibada : mashemasi watahusika na

- Kutayarisha kanisa ,kuisafisha na kupanguza viti ili viwe safi
- Kusafisha kisima na kuweka maji ndani
- Kutayarisha (kufua na kugoma) mavazi meupe ya ubatizo kufuatana na kimo, umri na unene wa wenye watabatizwa na ya wenye watabatiza

- Kutayarisha chumba ambamo mavazi yataweza kubadilishiwa mbele na baada ya ubatizo
- Kutayarisha wapi waimbaji watakaa, wapi wenye kubatizwa watakaa, wapi wazazi wa wenye kubatiza watakaa na kazalika.
- Kupanga viti na kuvitosha inje ikiwa ibada itafanyika inje kanisa

b) Wakati wa ubatizo

Kazi ya mashemasi ni ya :

- Kusaidia yule atakaye batizwa kuingia na kutoka katika kisima
- Kupanguza maji kwa sura na vichwa vya walio batizwa
- Kukaribisha watu wanao fika nyuma na kuwaongoza wapi watakaa
- Kuhusika na usalama wa wenye kubatizwa

c) Baada ya ubatizo

Mashemasi wanaitajika:

- Kukusanya, kufua, kugoma na kuchunga mavazi meupe yaliyo tumiwa kwa ubatizo
- Kuondoa maji ndani ya kisima, kukisafisha na kusafisha kanisa nzima
- Kurudisha kila kitu kunafasi yake
- Kuangalia nini iliweza kusaulika pembeni ya kisima, ndani ya kanisa na kufunga kanisa.

III. 3. Kazi za mashemasi katika ibada ya ndoa

Ibada ya ndoa ni mojawapo wa ibada za muhimu katika kanisa.
Umbalimbali na ibada nyingine, ibada ya ndoa ni ya furaha sana na inakusanya wakristo na wapagani; wenye kufuraiya ndowa na wenye wivu juu ya bwana ao bibi harusi pia wamefika. Ndio sababu utaratibu unaitajika sana katika ibada ya ndoa.
Kwa hivi kazi ya mashemasi itakuwa ya :

a) Mbele ya ibada

- Wanapashwa kutayarisha viti vingi zaidi kuliko siku zingine
- Kupanga viti wakitofautisha :
    - bwana na bibi harusi watakaa wapi
    - wazazi wa ndoa watakaa wapi
    - jamaa la bwana harusi litakaa wapi
    - wazazi wa bibi harusi watakaa wapi
    - waimbaji watakaa wapi
    - waalikwa mbalimbali watakaa wapi

- wachungaji wa kanisa watakaa wapi

- Kuhusika na kupanga gari za waalikwa na ile itakayo beba bwana na bibi harusi na kuchunga usalama wa gari zenyewe
- Kuchukua mpango kuusu:
    - nani atakaribisha bwana na bibi harusi na kuwaketisha katika ibada
    - nani atakaribisha waalikwa
    - nani atausika na usalama wa bwana na bibi harusi
- Kutafuta mauwa na kupamba kanisa
- Kutafuta na kuweka kanisani vitambaa mbalimbali vitakavyo itajika
- Kuzungumuza na kuelewana na wanamemba wa jamaa za bwana na bibi harusi kuusu utaratibu kanisani, katika karamu na kufaamu madaraka ya jamaa na ya mashemasi
- Kufaamu nani ata tamka hotuba ya protocol kati ya jamaa na kanisa
- Ikiwa karamu itafanyika kanisani , ni lazima mashemasi watayarishe vifaa vyote vya karamu(masaani, sabuni, vijiko, uma,n.k.)

c) Wakaiti wa ibada

Mashemasi:

- Watakaribisha na kuketisha watu, kila kikundi pa nafasi yake, katika kanisa
- kuhusika na utaratibu katika kanisa
- kuusika na usalama wa bwana na bibi harusi katika kanisa
- kurahisisha mawasiliano katika kanisa

d) Baada ya ibada

Kazi ya mashemasi ni:

- kulinda utaratibu wakati wa kuondoka kanisani : nani ataondoka wa kwanza , atafatwa na nani na atapitia kwa mlango gani
- kulinda usalama wa bwana na bibi harusi wakati wa kuondoka kanisani
- kuchunguza nini ilisaulika kanisani na kuilinda
- kusaidiana na jamaa za bwana na bibi harusi kwa kuongoza watu kujua wapi watakaa kwa kuchunga karamu
- kurudisha kila kitu kwa nafasi yake.

III.4. Kazi za mashemasi katika karamu

Karamu ni sherehe iliyo ya muhimu na ambayo kufaulu kwake ni mikononi mwa mashemasi. Mara nyingi manunguniko uingia kanisani kwa njia ya karamu. Imewapasa mashemasi kufanya huduma yao kwa

hekima ili watu wote wajisikie wamehudumiwa vizuri. Kwa hivi, washemasi wanaitajika kufanya kazi ifuatazo:

a) Mbele ya karamu

Mashemasi watausika na:

- Kutafuta chakula na vifaa ya karamu:
    - kujua chakula kitatoka wapi ?
    - kuvileta kwa gala
- kujuwa wanani watapiga chakula na ni watu wa aina gani
- kufaamu maitaji ya wale watakao piga na kuyatatua
- kutayarisha vifaa : masaani, vijiko,kopo, sabuni, tire-bouchons,n.k.
- kutayarisha vyumba vya kufanyia karamu: itakuwa fasi gani, watu wataenea ao hapana kuweka usafi, kupanga viti,
  kupamba chumba,n.k
- kutayarisha wanani watagawanya chakula.

b) Wakati wa karamu

Kazi ya mashemasi ni :

- Kuhudumia waalikwa
- Kuhusika na usalama wa watu na wa chakula
- Kusaidia waalikwa wanao itaji kwenda chooni
- Kuchunga utaratibu wakati wa kugawa chakula, kinywaji
- Kuleta hali ya furaha, amani na usalama kwa waalikwa
- Kufaamu nani anahuzunika, sababu gani na kumutunza kiroho
- Kujua nani amepata chakula na nani hajapata na kuwapatia chakula
- Kurahisisha mawasiliano ndani ya chumba cha karamu

c) Baada ya karamu

Mashemasi watahusika na :

- Kukusanya vyombo na vyakula vilivyo baki baada ya karamu
- Kuhusika na vyomba: kujuwa ikiwa kuna vilivyo potea, vilivyo vunjika; kuvihesabu
- Kusafisha vyombo na kurudisha kila kitu pa nafasi yake
- Kusafisha chumba cha karamu na kurudisha kila kitu pa nafasi yake
- Kutoa ripoti ya karamu kwa baraza la kanisa

III.5. Kazi ya mashemasi katika ibada ya meza ya Bwana

Meza ya Bwana ni ya lazima sana katika maisha ya wakristo; ndio sababu mtume Paulo anawaomba wakristo kuifanya kila mara wanapo kusanyika.
Shida kubwa ni kuona wakristo wengi wanakimbia wakati wa meza ya Bwana!

Mashemasi wanakuwa vilevile wa lazima kwa meza ya Bwana kupitika vizuri.Kwa hivyo, mashemasi wanaitaji kuelewa huduma yao na kuifanya kwa moyo safi ili watu wa Mungu wabarikiwe.
Kazi yao ni hii:

a) Mbele ya meza ya Bwana

- Kutafuta na kutayarisha vyombo vya meza ya Bwana
- Kufua, kugoma na kulinda vitambaa vya kufunika mkate na divai
- Kwenda kutafuta na kununua vifaa vinavyo itajika kwa meza ya Bwana
- Kupanga viti na, kutoa uchafu ndani ya kanisa baada ya ibada ya watu wote
- Kukaribisha na kuketisha watu katika ibada
- Kunawisha watumishi, watakao hudumiya wakristo, mikono

b) Wakati wa meza

Mashemasi wanaitajika kuketi na kushiriki meza ya bwana. Hii inamaanisha ya kwamba sio mashemasi wana hudumia kanisa kwa kugawa meza ya Bwana; hii ni kazi ya Wazee wa kanisa. Mashemasi wanaitajika kuketi na kungoja wahudumiwe sawa na wakristo wengine.

c) Baada ya meza

Kazi ya mashemasi ni:

- Kukusanya vifaa vya meza (mbirika,vikombe,vipande vya Mikate, vitambaa) kuvisafisha kugoma na kuvirudisha nafasi yake
- Kuondoa uchafu katika kanisa
- Kurudisha viti na meza, kila kitu pa nafasi yake
- Kusaidia watu kuondoka katika kanisa kwa utaratibu
- Kufunga milango ya kanisa.

IV.6. Kazi zingine za mashemasi

Sio tu katika ibada mbalimbali ndio mashemasi wanaitajika kufanya huduma yao; sababu pembeni ya huduma za kanisani, mashemasi wanaitajika kuhusika :
- Kusafisha ofisi ya kanisa na vitu vyote vilivyo ndani ya ofisi
- Kuhusika na kuchunga na kukinga masaani, vyungu,vijiko, makopo na vifaa vingine vya kanisa

- Kuhusika na kupokea, kupangisha na kuhudumia wageni kanisa
- Kuhusika na usafi katika lupango ya kanisa
- Kuhusika na kupanda na kutunza mauwa katika lupango yakanisa.

Hakika sio rahisi kuzungumuzia huduma na kazi zote ambazo Shemasi anaitajika kufanya kanisani katika kitabo; sababu :

- Yesu ndie Bwana wa kanisa na ni yeye anajua kila kundi na maitaji yake
- Kila zehebu inakuwa na utaratibu wake ya utumishi
- Ni Mungu ndie anapana karama na ni yeye anaelewa mahitaji ya wakristo
- Kila kanisa inakuwa na hali yake, vifaa vyake na maitaji yake ilio mbalimbali na ya kanisa zingine.

Basi, kwa yeye anaye tuita kumutumikiya na anaye tupatiya uwezo wa kumtumikiya ziwe sifa utukufu milee na milele , Amina.

Kwa mwisho

Katika kitabu hiki Kuhusu Huduma ya mashemasi katika Kanisa, tunatoka kuonyesha kwamba Mashemasi ni watumishi wa Mungu sawa na Wachungaji.

Pamoja na hiyo, tulitia mkazo kwamba si kila mukristo ndie anaweza kuombewa kuwa shemasi, sababu ina mubidi awe na mwito toka Mungu na awe na karama ya ushemasi. Kwa kufanya huduma yake vizuri, shemasi anaitajika kuwa na uhakika kuusu mwito wake, kuhudumia kwa unyenyeke, kufahamu tofauti kati ya kazi zake na za watumishi wengine kanisani na kuwa na hali na tabia zinazo pendeza Mungu na watu.

Kua na karama na mwito, haimuruhusu shemasi kuto kuheshimu utaratibu wa zehebu lake ikiwa inahambatana na Maandiko matakatifu. Sababu, pamoja na kutafuta kumupendeza Mungu, shemasi anawajibika kutii viongozi wa zehebu na Mchungaji wake.

Ni lazima pia shemasi aelewe umuhimu wa kushirikiana na makundi mengine ya watumishi kanisani kama : Mchungaji, wazee, waimbaji, kikundi cha wamama, cha wababa, cha vijana, watoto na kaza lika. Hii itasaidia kanisa kukomaa na kuongezeka kila mumoja akijihesabu kiungo cha mwili ambacho kinahaja na mwengine kwa kukomaa na kujisikia na furaha.